MARIE STOPES
TANZANIA




# NGUVU YA UTASHI:
# JARIDA LA ROBO MWAKA LA MARIE STOPES TANZANIA

> “Serikali inatambua haja ya kushughulikia hitaji ambalo halijafikiwa la Uzazi wa Mpango na kuhakikisha wanawake na wasichana wanapata huduma baada ya mimba kuharibika bila unyanyapaa. Huduma hizi ni huduma tunazozipa kipaumbele sana katika mipango yetu.”

Dk. Mzee Nassoro, Mkurugenzi Msaidizi - Mkurugenzi Msaidizi kitengo cha Afya ya Uzazi, Wizara ya Afya.

Tunapomaliza robo tatu ya mwaka (2023), tunafuraha kukushirikisha maendeleo na matokeo ya kazi zetu. Kujitoa kwenu na mchango wenu katika kuihudumia jamii kumekuwa muhimu katika kuendeleza dhamira yetu. Shukrani zetu za dhati ni kwa washirika wetu ikiwa ni pamoja na serikali, kwa kuhakikisha jamii inapata huduma za afya ya uzazi kwa kuzingatia utashi.

Katika kukabiliana na changamoto ambazo hazikutarajiwa ikiwa ni pamoja na kupungua kwa usaidizi kwenye eneo hili la afya ya uzazi. MST imeendelea kukabiliana, kuvumbua, na kuendelea kutoa huduma za afya ya uzazi .

Tumeendelea kuwa imara katika kuwawezesha watu binafsi na kuimarisha sekta ya afya ya umma, kukuza eneo la Elimu ya afya ya uzazi, kushawishi mabadiliko ya sera ili kuhakikisha tuna dunia ambayo watu wote wanaweza kupata haki za afya ya uzazi kwa heshima na uhuru.

Ni ndani ya robo hii ya Mwaka ambapo tuliadhimisha siku muhimu za Kimataifa kama vile Siku ya Vijana, Siku ya uzazi wa mpango na Siku ya utoaji mimba usio salama. Maadhimisho haya yote ni muhimu ili kutambua umuhimu wa kuwapa watu uamuzi wa kuchagua njia za afya ya uzazi ili kuwapa fursa ya kufanya maamuzi sahihi kuendana na hali na matarajio yao.

## Matokeo ya Kazi zetu Robo ya Tatu ya Mwaka

**472K**
Jumla ya wateja waliofikiwa

**79K**
Vijana walio chini ya miaka 20 (18% ya wateja wote waliofikiwa na huduma ya uzazi wa mpango ni vijana walio chini ya miaka 20).

**1.4M**
Alama za muda wa uzuiaji mimba zilizozalishwa

**716K**
Mimba zisizotarajiwa zilizoepukwa

**923**
Vifo vya akina mama vilivyoepukwa

**206K**
Utoaji mimba usio salama uliepukwa.

# MATUMIZI YA VYOMBO VYA HABARI KATIKA KUENDELEZA UTASHI KWENYE MASUALA YA **UZAZI WA MPANGO** NCHINI TANZANIA

Ili kuhakikisha upatikanaji wa taarifa, tulitumia vyema kampeni ya kidigitali na vyombo vya habari kwa kutumia dhima mbalimbali kama #MaamuziSmati na #AfyaYakoHatmaYako kwa lengo la kukuza kipaumbele cha masuala ya Uzazi wa Mpango na huduma baada ya mimba kuharibika nchini Tanzania. Kupitia kampeni hii, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na shirika la habari la mwananchi katika kuadhimisha siku ya kimataifa ya uzazi wa mpango duniani tuliweza kufanya mjadala kupitia mtandao wa X Space uliowaleta pamoja wasikilizaji na wachangiaji 480 ambayo iliwezesha kuwafikia takribani watu milioni 2.5.

Katika mjadala huo masuala mbalimbali yaliibuliwa ikiwemo kuruhusu upatikanaji wa njia za uzazi wa mpango za dharula bila kipingamizi kwenye maduka ya dawa, ambapo Mratibu wa Kitaifa wa Uzazi wa Mpango, Bi. Zuhura Mbuguni aliwahakikishia washiriki kuwa Wizara ya Afya na MST zinashirikiana kikamilifu kufanya tathmini kuhusu masuala ya upatikanaji wa njia za uzazi wa mpango za dharula kwenye maduka ya dawa. MST itaendelea kuendesha kampeni ili kuondoa dhana potofu kwenye matumizi ya njia za uzazi wa mpango na kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za masuala ya afya ya uzazi na kushawishi kuwepo kwa mazingira wezeshi ili kuhakikisha huduma za afya ya uzazi zinapatikana kwa kwa utashi.



Timu ya Madaktari wa MST kutoka kushoto: Dk. Emmanuel Kimario, Dk. Seleman Mbyallu, Dk. Judith Mashalla, na Dk. Robert Shokolo

## Madaktari wahudhuria Mkutano wa 55 wa Kisayansi wa Kitabibu

Hivi karibuni Marie Stopes Tanzania (MST) ilishiriki katika Mkutano Mkuu wa 55 wa Kisayansi na kitabibu wa Chama cha Madaktari Tanzania, ulioshirikisha wataalamu wa matibabu, watafiti na wadau mbalimbali katika mijadala muhimu kuhusu sekta ya afya ya Tanzania.

Mkutano huu ulitoa fursa ya kushughulikia changamoto mbalimbali ndani ya sekta ya afya.
Madaktari hao walijadili hitaji la dharula la kushughulikia maswala ya ubora wa huduma yaliyoonyeshwa na tafiti za hivi karibuni na kusisitiza jukumu muhimu la Wafanyakazi wa Afya ya Jamii katika kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kwa ubora wa juu kwa Watanzania wote. Timu ya Madaktari kutoka MST walioshiriki katika mkutano huo ni pamoja na Dkt. Selemani Mbyallu (Msimamizi wa ubora huduma za afya) Dkt. Emmanuel Kimario (Msimamizi wa Hospitali), Dk. Robert Shokolo (Meneja wa Ubora huduma za afya), Dk. Judith Mashalla (Mratibu wa ubora huduma za afya), na Dk. Mashingo Lerise (Meneja wa Hospitali ya afya ya uzazi Mwenge).

## Washirika wa mradi wa Afya kwa Vijana (YouthforHealth) wajumuika kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Vijana

MST yaungana na washirika wengine kuadhimisha siku ya vijana duniani mkoani Dodoma. Maadhimisho haya yaliwaleta pamoja washiriki zaidi ya 1,000 kutoka mashirika 40 ya ndani na kimataifa. Katika kuadhimisha siku hii kulikuwa na maonyesho yaliyolenga dhima mbalimbali ikiwemo: mifumo ya kitaifa ya masuala ya maendeleo ya vijana, afya na jinsia ikihusianishwa na mabadiliko ya tabia nchi, katika kuwawezesha vijana kiuchumi. Katibu Mkuu, Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu wa Tanzania, Profesa Jamal A. Katundu, alikuwa miongoni mwa waliohudhuria.

Wawakilishi wa mradi wa Afya kwa vijana walishiriki katika mijadala kwa kushirikiana na wadau wengine ikiwemo wawakilishi kutoka Wizara ya Afya, Amref, na UNFPA ambapo walijadili masuala ya afya ya uzazi. Tukio hilo lilihitimishwa kwa maonesho ya awamu ya pili yaliyoongozwa na vijana ambapo vijana 400 walipata huduma na taarifa mbalimbali.

# Kufikia wateja wengi huku tukidumisha ubora, ufanisi na kujenga uwezo kwa watoa huduma wa serikali

## Changamoto


Mnamo mwaka 2018, Wizara ya Afya ilipitia muongozo wa uzazi wa mpango wa huduma za mikoba ambapo iliweka kikomo kwa utoaji wa huduma za njia za uzazi wa mpango za kudumu kutolewa kwenye hospitali au vituo vya afya vyenye vyumba vya upasuaji tu. Hii kwa namna fulani iliathiri utendaji kazi kwa wadau wengi wanaotekeleza miradi ya uzazi wa mpango na utendakazi wa huduma hizi ulipungua nchini.

Kiongozi wa Uhamasishaji wa MST anasema, “Uamuzi huo ulituathiri sana. Ilikuwa vigumu kutoa huduma kama tulivyokuwa tukifanya hapo awali, gharama zilikuwa kubwa sana kwa mteja mmoja kwa vile huduma hiyo ilihusisha kumsafirisha mteja kwenda na kumrudisha kutoka kwenye kituo kisicho na chumba cha upasuaji hadi hadi kituo ambacho kina chumba cha upasuaji. Utaratibu huo ulihatarisha kutowafikia wateja wengi waliohitaji huduma.

## Suluhisho

Baada ya kufanya uchambuzi wa gharama na faida, kusoma mazingira ya kazi na kushauriana na serikali, mwaka 2019 shirika liliamua kufanya majaribio ya timu za uhamasishaji kufanya kazi katika vituo viwili kwa siku moja ambapo timu moja inagawanywa katika sehemu mbili. Kituo kimoja kinaweza kikawa au kisiwe na chumba cha upasuaji. Muundo wa timu pia ulibadilika na kuwa na wafanyakazi wanne wa MST na wawili wa serikali ambapo daktari wa upasuaji hupangwa sehemu ambapo njia za Uzazi wa Mpango wa kudumu zinaweza kutolewa.

Timu husafiri pamoja kwa kutumia gari moja na vitengo vidogo vidogo huachwa katika sehemu zinazotakiwa (mara nyingi pakiwa na umbali wa kilometa 30 kati ya kituo). Kila kituo kikisaidiwa na mfanyakazi wa kujitolea katika kijiji huku matangazo yakitolewa kupitia mfumo wa matangazo ya umma na pikipiki wakati wa kipindi cha kazi.



Mfumo wa Huduma za Mikoba MST

## Matokeo

Kutokana na uchanganuzi wa ufafanuzi wa sehemu mbalimbali na mahojiano ya kina yakilinganisha timu zilizogawanyika na za kawaida zinazofanya kazi kwa siku moja, mfumo wa timu uliogawanyika umeonekana kutoa huduma zinazofikia maeneo mengi zaidi, zikiwafikia wanawake wengi zaidi wenye mahitaji makubwa ya huduma za Uzazi wa Mpango. Kwa timu zilizogawanyika zinazofanya kazi kwa siku moja, wastani wa idadi ya wateja wa Uzazi wa Mpango iliyofikiwa kwa siku imeongezeka kwa asilimia 35 ikilinganishwa na muundo wa kawaida.


MARIE STOPES TANZANIA

Kitalu 421&422 Mwenge, Kijitonyama
SLP 7072.
Dar es Salaam, Tanzania
T: **+255 22 227 4991**
**Tupigie Bure: 0800753333**
Barua pepe: info@mst.or.tz

mariestopestz
@MarieStopesTZA
@mariestopestz
marieStopes Tanzania